

Muhtasari wa Kufundisha kama Kristo

Fokasi kwa Yesu Kristo

| Fundisha kuhusu Yesu Kristo Bila Kujali Kitu Unachofundisha | Wasaidie Wanafunzi Kuja kwa Yesu Kristo |
|---|--|
| Sisitiza Mfano wa Yesu Kristo | Wasaidie Wanafunzi Kutambua Upendo, Nguvu na Rehema za Bwana katika Maisha Yao |
| Fundisha kuhusu Majina, Wajibu, na Sifa za Yesu Kristo | Wasaidie Wanafunzi Kuimarisha Uhusiano Wao na Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo |
| Tafuta Alama Ambazo Hushuhudia juu Yesu Kristo | Wasaidie Wanafunzi Kwa Makusudi Kabisa Wajitahidi Kuwa Zaidi kama Yesu Kristo |

Kanuni za Kufundisha Kama Kristo

| Wapende Wale Unaowafundisha | Fundisha kwa Roho | Fundisha Mafundisho | Alika Kujifunza kwa Bidii |
|--|--|---|--|
| Waone wanafunzi katika njia ambayo Mungu anawaona. | Jiandae mwenyewe Kiroho. | Jifunze mafundisho ya Yesu Kristo kwa ajili yako mwenyewe. | Wasaidie wanafunzi kuwajibika kwa kujifunza kwao wenyewe. |
| Tafuta kuwajua— kuelewa hali zao, mahitaji yao na nguvu zao. | Daima uwe tayari kujibu misukumo ya kiroho kuhusu mahitaji ya wanafunzi. | Fundisha kutoka katika maandiko na maneno ya manabii wa siku za mwisho. | Wahimize wanafunzi kuja kumjua Mwokozi kwa kujifunza injili kila siku. |
| Waombe kwa majina. | Tengeneza mazingira na fursa kwa ajili ya wanafunzi kufundishwa na Roho Mtakatifu. | Wasaidie wanafunzi kutafuta, kutambua na kuelewa kweli katika maandiko. | Waalike wanafunzi kujiandaa kujifunza. |
| Tengeneza mazingira salama ambapo wote wanaheshimiwa na kujua michango yao inathaminiwa. | Wasaidie wanafunzi kutafuta, kutambua na kutenda juu ya ufunuo binafsi. | Fokasi kwenye kweli ambazo zinaongoza kwenye uongofu na kujenga imani katika Yesu Kristo. | Wahimize wanafunzi kushiriki kweli wanazojifunza. |
| Tafuta njia sahihi za kuelezea upendo wako | Shuhudia kila mara, na kuwaalika wanafunzi kushiriki hisia zao, uzoefu wao na shuhuda zao. | Wasaidie wanafunzi kupata uhusiano binafsi katika mafundisho ya Yesu Kristo. | Waalike wanafunzi kuishi kile wanachojifunza. |